# Gazeti la Kimataifa
## Waabuduo Damu ya Kristo

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

…Kwa Neno Lako…

Lima, Peru 5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 1, Januari 2019


Mhariri

## Wahudumu – Wajenzi – Wahuishaji

Wachungaji walienda na kumkuta Mtoto aliyevalishwa nguo akiwa amelazwa kwenye hori la kulishia wanyama!

Nani anajua nini walichokuwa wamekisema! Kukata tamaa na kutoridhika au kushangazwa na kudhihakiwa?

Kwa kuwa mjumbe huyo alikuwa amewasumbua katikati ya usiku. Hakuwa mchokozi wa kwanza usiku, na kwa hakika atakuwa mchokozi wa mwisho.

Labda wachungaji watakuwa walifikiria ni habari za udanganyifu, kama za wanawake au za jambo fulani, ili kutoka nje ya dimbwi na harufu mbaya ya wale kondoo ambao mpaka siku hiyo walikuwa wametoa wasifu wa maisha yao. Badala yake ... habari ya mtoto na familia ya waombaji kutoka familia nyonge.

Kitu gani alitaka kutoka kwao huyo mtoto aliyezaliwa katika uzio wa ulimwengu uliotapakaa vurugu na ugaidi?

Jambo moja: kutoka katika mantiki ya kutojali na ile ya utofauti. Kwa kifupi, aliwaomba kuwa watumishi wa wanadamu waliokata tamaa, wajenzi wa jamii iliyoraruliwa na wahuishaji wa makanisa na jumuiya zilizonyimwa heshima.

Kuwa Wakristo na wenyeji wa dunia, ambamo huishia kwenye kuwalinda wadogo na kutekeleza mipango ya amani na mshikamano. Jukumu kubwa lilikabidhiwa kwao: **Wanasiasa wasiofaa (wasiowaaminifu) wanaitwa kufanya kazi kwa faida ya wote,** wakishinda tamaa zao za maslahi binasfi na kukuza haki za watu si kubaki kuwa wachungaji wa kondoo, bali kuwa wachungaji ambao husikia sauti na milio hata kama iko mbali.

Watumishi, wajenzi, wahuishaji wa nyumba ya pamoja, wa heri nane zinazohamasisha ushiriki wa vijana, wasiopokea mikakati ya hofu na vita na ambao hufanya upendo kama njia dhahiri ya nyumba ya pamoja na siyo ya sarafu ya pamoja – kama anavyosema Don Tonino Bello, mahali ambapo kila mtu anaweza kuishi na siyo kuishi zaidi.

Hapa ndipo hububujika kwa ajili ya wachungaji wapya ya milenia ya tatu, wanaosumbuliwa wakati wa usiku wa Noeli, mbinu mpya ambazo ni elimu kwa watawala na kwa wananchi wenye wajibu, ambapo Padre Milani amejenga shule, mwelekeo unaohitajika kwa ajili ya kurejesha heshima kwa watu, ambayo iliibwa na kutoa kipaumbele kinachostahili na halali kwa wale wanaoendelea kuamini kwamba maisha ni zawadi tu.

Hakuna mtu aliyeachwa nje ya mradi huu wa amani ili kuendesha siasa sisizo na ubaguzi kama zile zilizofanywa na Mtakatifu Maria De Mattias.

***Sr. Mimma Scalera, ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- Wahudumu – Wajenzi – Wahuishaji 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- …Mabadiliko yanayozaa uhai… 2
- Hija ya Kina 3

*Toka Ulimwengu ASC*
- Habari kutoka Liberia 4
- Huduma ya Elimu Msumbuji 5
- Kutafuta wenye Vipaji 6
- Ildegarda Nabii 7
- Kongamano la Tatu la Watawa Vijana: Huru katika Roho Mtakatifu 8

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Elimu kwa heshima ya viumbe vyote 9

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 11
- Sherehe za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha 11
- Waliorudu Nyumbani kwa Baba 11

# … Mabadiliko yanayozaa uhai…

... ni maneno ya nembo ya mkutano wa Halmashauri Kuu Iliyopanuka iliyokutano kuanzia tarehe 21 hadi 30 Novemba 2018, kwenye Nyumba Kuu, ikiwa na ASC wanaowajibika na Region na Faundation kutoka kila sehemu ya dunia.

Ndani ya siku kumi, pamoja na ajenda yenye utajiri iliyobeba maudhui muhimu kwa ajili ya Shirika na kwa ajili ya kila mwabuduo kwa namna ya pekee, tulitafuta kwa pamoja **" NJIA ZA MABADILIKO"**



Kwenye ufunguzi wa mkutano wa Halmashauri, Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika alituhimiza kukumbatia mchakato wa mabadiliko akitukumbusha kuwa mabadiliko ni moja ya mwaliko muhimu sana ambao unasindikiza kwa namna inayofaa kila maamuzi yaliyofanywa wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka 2017 na alituuliza swali muhimu: Kama Shirika tunaelewa nini tunapoongea juu ya mabadiliko?!

Siku kwa siku tuliweza kuwa wazi zaidi kuelekea njia mpya, tukishirikisha mang'amuzi na kufahamiana kwa kiasi kikubwa kupitia mawasilisho kutoka kila mazingira halisi, madogo na makubwa, yaliyoonekana kama "puzzle" ya picha moja ambayo ni Shirika.

Kama Uongozi Mkuu, tulishirikisha matarajio na hatua halisi zilizotekelezwa kuhusiana na utume tuliopokea kutoka Mkutano Mkuu 2017, na tuliwasilisha mpango wa miaka sita juu ya mada: "... Ule mpango mzuri wa vitu..." iliyogawanyika katika maeneo matano kama mtazamo mmoja ambao unalenga mbali zaidi ya shughuli moja moja:

- Maeneo ya miito/mialiko ya kinabii
- Maeneo ya kukutana sisi kwa sisi
- Maeneo ya mashirikisho yanayozaa (ofisi ya uchumi)
- Eneo la ujengaji wa umoja (ofisi ya katibu)

Wajumbe wa Halmashauri Kuu Iliyopanuka walifanya kazi katika makundi kuhusu mada zilizowasilishwa, wakisimama zaidi ya yote juu ya baadhi ya hoja: maandalizi ya Novisiati ya Shirika, marekebisho ya Sheria Zetu, njia zinazowezekana kwa ajili ya Foundations na Region zenye mazingira magumu, mipango ya CIS, ya JPIC na tathimini ya VIVAT.

Wawezeshaji wawili, Dr. Rosanna Virgili na Sr. Maria Cristina Avàlos SSpS pamoja na Padre Leonello walitusaidia katika kazi ya utafiti wa njia mpya za mabadiliko: Rosanna, alitusogeza karibu na vipengele vya Biblia na tasaufi ya mabadiliko, Sr. Maria Christina, alituelezea juu ya hoja zinazohusiana na Sheria zetu za Shirika.

Hija kuelekea Vallecorsa na Acuto ilitufanya tujisikie mahujaji kwa kiasi kikubwa katika safari juu ya karama yetu ili tutambue tena umuhimu na uzuri wa kuwa tumebadilishwa kweli.

... Safari yetu ya mabadiliko inaendelea..., na kwa ajili ya ukumbusho tulipokea kimtungi kidogo cha udongo, ishara ya mchakato wa mabadiliko ambayo tunaitwa kuyaanza kwa uwajibikaji na uwazi wa moyo.

Kila mmoja alirudi katika mazingiea yake kwa ujumbe: "Nena na ukawe mabadiliko yanayozaa uhai ulimwengungu".

***Sr. Matija Pavić, ASC***



# Hija ya Kina …

## Juu ya nyayo za Maria De Mattias kwa ajili ya mabadiliko ya uhakika ya moyo

Mnamo Novemba 24, wakati wa mkutano wa Halmashauri Kuu Iliyopanuka, wajumbe walifanya safari kuelekea Vallecorsa na Acuto ili kusafiri tena na Maria De Mattias katika kina cha Upendo unaoita, unaoshawishi na kubadilisha. Hapa, kati ya milima mitupu na vilima vikali, Mungu alianza mchakato wake wa uongofu ndani yake. Siku hiyo ilihaishwa na kuongozwa na Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, na Sr Manuela Nocco.

Pamoja na hali ya hewa ya mvua, kwa kawaida mvua za vuli, hamu ya kukutana na Maria De Mattias katika nyakati muhimu za historia yake, maneno yake, safari yake ya imani, ambayo tunaweza kupata nguvu, mafundisho na ujasiri, haikupungua.

Katika hatua za kutoka Roma kwenda Vallecorsa na Acuto, Mwanzilishi anashuhudia kwamba mabadiliko ya kweli yanapatikana kwa njia ya kukaribisha Upendo. Kwa kweli, utukutu wake wa ujana unakuwa fursa ya kutafuta zaidi. Mungu alielewa mateso yake na Maria de Mattias akaruhusu kugeuzwa kutoka ujana mtukutu kuelekea kuwa mwanamke mwenye upendo na ujasiri.

Hii inatuonyesha jinsi Upendo unavyokuwa msukumo usiochoka wa kutoka nje ya nafsi ili kukaribia daima kwa kasi kwenye moyo wa Mpendwa. Kwa kufuata hatua zake kutoka Kanisa la Mtakatifu Martin, ambako alibatizwa, pale aliposikia wito wa kumfuata Mwana-Kondoo, mpaka kutoka kwenye Mlango Missoria, inaamsha tena mchakato wa upyaisho usiokoma, wa uongofu ambao unajua maneno ya kina zaidi. Majibu makubwa zaidi ya kujihusisha, ambayo huomba kila wakati kuacha kitu nyuma ili kupunguza uzito wa mzigo kuelekea ule mpya wa kukumbatia na kuishi. Siku ya kutafakari ilimalizika na liturujia ya Ekaristi.



Na hivyo Acuto, mahali ambapo kwa Maria ilikuwa mahali pa utekelezaji wa ahadi, lakini pia unabii wa maisha yanayoendana na Injili. Akiongozwa na upendo, Maria akawa mtangazaji wa mipango ya Mungu katika historia na ya Utendaji Wake kwa ajili ya wokovu wa watu.

Kwa hiyo, wahujaji wa Mkutano wa Halmashauri Kuu Iliyopanuka 2018 wanaendelea kujiuliza kuhusu kile ambacho Bwana anatutaka sisi kukiacha ili kukaribisha mabadiliko. Anatuuliza maswali kuhusu nchi ambazo tunaishi na juu ya yote ni upeo gani tumepata ili kufanya utafiti na zaidi ya yote upeo kuelekea pale macho yetu yanakoweza kufikia.

Leo Maria De Mattias anaendelea kuwa ushuhuda wa mchakato ule ambao tunaitwa kushiriki. Mchakato ambao ni jibu la uaminifu wetu kwa Mungu, kwa Roho wake na kwa historia Yake, ambao hatuwezi kuukwepa.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

Eneo la Bara: Africa
Misioni Liberia

# Habari kutoka Liberia:
## Kutoka habari binafsi za Therese Wetta, ASC

**Novemba 29, 2018**

Leo tarehe 29 Novemba, hapa Laberia ni sikukuu ya kitaifa, kwa heshima ya Rais aliyemaliza muda wake. Chuo kikuu cha Tubman, kituo chetu cha jimbo kikiwa mbali mwendo wa saa mbili kutoka hapa, kina jina hilohilo. Kwa hiyo tunasherehekea kama siku ya shukrani, tukionja vyakula vitatu vya aina yake: wali, siagi ya nazi (kiungo cha nazi ambacho kinanyunyiziwa juu ya wali) na nazi mbichi. Alhamisi iliyopita tulipika pasta kwa ajili ya chakula cha mchana.

Ijapokuwa ilikuwa siku ya sikukuu, asubuhi yake Sista Zita alipata wanawake watano kwa ajili ya kuwafundisha ushonaji. Likizo hapa hazitofautiani na siku zingine hapa, ukiacha siku ya jumapili. Wanawake ni waaminifu sana kwa kuja kuhudhuria somo.



Kwangu, sikuwa na shule! Asubuhi niliamukia kwenye kichuguu cha mchwa ambacho urefu wake kutoka sakafuni ulifikia fremu ya mlango ambao uko kati ya chumba changu cha kulala na bafu ambacho hakikuwepo usiku uliopita, tulitumia dawa ya kuua wadudu na maji ya moto kwa kukitoa. Tunaishi kwa tatizo hili la mchwa ndani ya nyumba kwa sababu ya nguzo za miti za kuta ndani na nje. Hali hii ilitufanya tuelewe kuwa tungeweza kuosha madirisha kwa sababu kipindi cha mvua kilikuwa kimemalizika.

Wakati nilipokuwa nafanya usafi mkuu kwenye chumba changu, nilikuwa nafikiri kipindi cha Majilio sasa kiko mlangoni na mwaka mpya wa liturjia unaoanza. Nilifikiri labbda ingekuwa vigumu zaidi kusafisha moyo wangu kulinganisha na dirisha au sakafu. Tunahitaji kusaidiana kujiandaa kwa kipindi hiki kitakatifu kuleta matunda yanayotamaniwa.

Wiki hii, watoto sita wa darasa la nne, kwa kukataa kufanya mtihani walikuwa wameadhibiwa na mwalimu ambaye aliwataka waondoe mapambo yote na kusafisha kanisa, na wanafunzi wengine wa darasa la tano kwa hoja hiyohiyo walitakiwa kuosha mabenchi ya kanisa. Sasa kanisa tayari kwa mwaka mpya wa liturjia!

Wiki hii pia nilipata uzoefu mwingine wa safari, wakati nilipokuwa nakwenda Pleebo kwa pikipiki (saa tatu na dakika 15 kwenda na wakati huo huo kurudi). Hakukuwa na dereva wa kuendesha gari yetu na barabara ilikuwa bado na matope kutokana na mvua, hivyo hatuwezi kuendesha wenyewe. Dereva wa pikipiki ni mwanaparokia ambaye alinihakikishia usalama na mimi nilijisikia salama, hasa pale nilipotoka kwenye gari na kutembea kwa miguu kando ya kilima, ili kuanza safari ya kurudi, miguu yangu bado ilikuwa inazungumza. Kulikuwa na matope sana kwenye kingo za barabara lakini nilipaswa kwenda benki kwa ajili ya kuchukua hela. Sasa tumeanzisha mpango ambapo safari kama hii haitakuwa ya lazima tena. Baada ya dakika 45 toka niliporudi nyumbani mvua ya mawe ilianza ikiwa na ngurumo na radi, hali ya hatari sana kuwa kwenye pikipiki katikati ya savannah. Dereva hakuweza kujua kwa nini mvua ilikuwa inanyesha kwa nguvu sana.

Wiki ijayo yataanza majaribio ya awamu ya pili ambayo yatafanyika mfululizo kwa wiki sita. Nasali ili mashine ya kutoa nakala ifanye kazi ili kuweza kutoa nakala badala ya kuandika majaribio kwenye ubao. Likizo ya Noeli inaanza tarehe 21 Disemba hadi tarehe 3 Januari.

Nawatakia nyote tafakari njema ya Majilio yenye mafanikio, wakati tukiungana katika sala na katika upendo.



# Huduma ya Elimu Msumbiji

Moja ya ndoto za Mt. Maria De Mattias ilikuwa ile ya kuelimisha watoto, wasichana na wanawake wa jamii ya wakati wake. Ndoto hii bado inaelelea kupitia huduma ya elimu inayotolewa na Waabuduo wengi katika sehemu nyingi duniani, ili kuwapa watu heshima.

Masista waabuduo watanzania huko Msumbiji wanashirikiana na Parokia ya Mt. Frumenzio ya Roma. Kwa pamoja wanasaidia kutoa huduma ya elimu kwa watoto kwenye shule za chekechea za Goba, Bakabaka na Mt. Frumenzio iliyoko Mefuiane. Shule ya Goba ina watoto 68, ya Mt. Frumenzio ina watoto 108 na zote mbili zinaongozwa na Sr Yohana Amu, ASC, wakati shule ya Bakabaka, inayoongozwa na Sr. Flaviana Alfredy, ASC, ina watoto 83.

Kuanzia tarehe 7 hadi 9 Novemba 2018 baadhi ya watoto wa shule hizi walihitimu masomo ya shule ya chekechea: watoto 48 wa shule ya Mt. Frumenzio, 28 wa shule ya Goba na 37 wa shule ya Bakabaka.

Watoto wa shule hizi tatu wamejifunza kusoma, kuandika na hata tunu njema za maadili na wamekuwa katika msingi mzuri wa kuweza kuendelea na elimu ya msingi na kuendelea kujiandaa ili kuwa raia wema wa wakati ujao.

Wakati wa mahafali yao, watoto walitoa shukrani zao kwa masista na walimu wao kwa utayari wao wa kuwasaidia katika masomo yao.

Elimu ni muhimu kwa jamii ya Msumbiji ili kuweza kuwasaisia kuondokana na matatizo hasa vita ya wao kwa wao ya muda mrefu. Sisi tunaamini kuwa elimu tunayotoa kwa watoto itakuwa chachu ya mabadiliko ambayo itakuza upendo na haki katika nchi. Kwa kuwa hizi ni tunu msingi za kurudisha amani iliyopotea.

Malezi waliyopokea watoto yatawaweka katika kiwango cha kuwafanya wajenge nchi na heshima yao.

***Sr. Yohana Amu, ASC***



Sista Yohana, Walimu na watoto wa shele ya chekechea Goba



Sr Yohana, Walimu na watoto wa Shule ya Mt. Frumenzio



Watoto wanacheza wakati wa burudani

# Kutafuta wenye Vipaji

Katika jamii ambayo tunaishi zaidi kwa kutafuta kuridhika mara moja na kutaka “kukomesha” matatizo kwa haraka, jamii ambamo hakuna “pumzi pana”, hamu na uwezo wa kufikiria na kujenga ni maamuzi ya makubaliano mapya kati ya utamaduni na tamaduni ambazo zinaweza kuelezea mtazamo wa ubinadamu mpya. Kwa mtazamo huu, katika siku za tarehe 16-17 Novemba 2018, huko Trani, katika kituo cha kiroho cha “Sanguis Christi” kulikuwa na SEMINA YA MIPANGO iliyoongozwa na Sr. Mimma Scalera, mtaalam wa mipango, na kuwa na mada “Kutafuta watu wenye vipaji”.



Lengo la semina lilikuwa ni kuwaelezea washiriki mbinu na njia muhimu kwa ajili ya uwasilishaji wa miradi na kuwapa mtazamo wa mpango mpya wa Fedha kwa kipndi cha miaka 2014 -2020 na vipaumbele vya Agenda ya Siasa ya Jumuiya ili kujiweka wenyewe kwenye mipango ya Ulaya na taifa . Lengo kwa hiyo, lilikuwa kuandaa nafasi zinazoonekana kwa ukuaji wa ujuzi, kupitia kuimarisha ujuzi msingi na kupata ujuzi mpya na wa pekee. Wakati wa kozi, mada kama vile mradi wa mzunguko wa maisha, utekelezaji wa miradi, usimamizi na tathimini, mpangilio wa fedha na uundaji wa ushirikiano zilifundishwa kwa kina. Kesi za udanganyifu zilielezwa na washiriki, masisita wa mashirika mbalimbali, na walei wanofanya kazi parokiani, kwenye vyuo vya ufundi, katika idara za kijamii na tamatuduni. Semina iligawanyika katika vipindi vya mafunzo kinadharia na kivitendo, ikiruhusu ufanisi wa shughuli ya mafunzo ambayo yanahamasisha uwajibikaji wa wote, kwa njia ya ushiriki na mbinu ya mwingiliano ambayo iliruhusu uwezekano wa kufungua nafasi ya mazungumzo kati ya washiriki na mkufunzi.




Semina ilimalizika kwa matashi mema na wajibu katika kushinda ubinafsi na utendaji nusunusu wa kazi zetu za kichungaji na kuingiza mifumo mipya ya pamoja kwenye kiini cha “utendaji wa pamoja” ili kukuza uinjilishaji katika tamaduni za leo.

***Sr. Anna Grazia Di Liddo, ASC***

# Ildegarda nabii

Ildegarda nabii ni jina la mwenye hekima ambalo Prof. Neria De Giovanni alilitangaza mwaka mmoja uliopika ili kusimulia historia na tabia ya huyu Mtakatifu. Tangu tarehe 7 Oktoba 2012 Papa Benedicto alipomtangaza kuwa Mwalimu wa Kanisa, huyu mwanamke alijieleza mwenyewe.

Kutoka Castelplanio alifika mwenyewe De Giovanni akiwakilishwa na zaidi ya watu mia, waliovutiwa na tunu za mwanamke wa zama za kati ambaye bado anatoa mwanga na maana ya maisha ya leo. Kulikuwa na Kituo cha Kiroho "Juu ya Mlima", kilichohuishwa na wanawake, watawa Waabuduo watatu wa Damu ya Kristo, ambao wanajitoa kwa muda tofauti kwa kuwatambua wanawake na tunu zao katika Kanisa na katika jamii.



Sura ya huyu mtakatifu na mchaji ni mwito kwetu sisi sote, kama "Laudato si".

Tunaona kwa urahisi kwamba baadhi ya mahubiri na maelekezo, au katekesi, hutofautisha dhahiri tunu za maadili na na za kiroho, kutufanya kuwa makini kwa zile za mwanzo Je! Zipi ni tunu za maadili? Inawezekana kudharau uzuri na mpangilio wa mwili, mavazi, mchezo na muziki, majani yanayoponya na kila kitu kinachohusu afya na usawa wa uwepo kwa binadamu? Ni dhahiri kwamba vinaweza daima kuwa vitu vya kutumia. Lakini kuwa makini usitenganishe. Hapa ni Ildegarda, Abate wa monasteri ya Bingen, ambaye alifariki akiwa na umri wa miaka 81 mwaka 1179, mwanamke mwenye utajiri wa maarifa ambaye anapenda kujifunza sayansi ya asili na dawa, pamoja na usafi na lishe ya binadamu. Katika Zama za Kati mwanamke mchaji, ambaye anapenda dunia na mimea yake, ambaye anapenda kuimba na kuwafanya watawa wake wacheze kwa furaha na shangwe, ni ishara nzuri kwetu pia. Ni za ajabu hizi monasteri ambazo zinapenda uhai, ardhi, na kwa pamoja wanaishi katika ushirika na Mungu kila wakati.

Leo inazaliwa tena roho fulani ambayo "huchomoza" kutoka katika historia na kwa hiyo kutoka kwenye mwili na kutoka katika huduma yake na uzuri wake. "Wao husali sala ndefu ili kuonekana na watu" aliongea Yesu kuhusu matajiri kwenye uwanja wa hekalu. "Wao hufunga mara nyingi", aliongea Yesu kuhusu Mafarisayo. Sanamu hazigombani, hazikiimbi, bali huchochewa ndani na moto wa Roho Mtakatifu Paulo kwa Wagalatia sura ya 5 anatofautisha matunda ya Roho na matunda ya mwili. Haya siyo kitu kingine isipokuwa udhaifu, kama Papa anavyopenda kusema, hakuna kitu kingine ila ubinafsi uliojifunga ndani wenyewe.

Ildegarda alipata zawadi ya maono na ya unabii. Aliishi katika kipindi cha historia ambacho Kanisa na utawala wa kipapa havikuwa vya kienjili. Alitoa sauti ya kinabii kwa maaskofu na kwa Papa. Aliandika "Laudato Si" kabla ya nyakati, akihangaika kulinda ardhi na matunda yake kwa ajili ya manufaa ya binadamu, ya kila mtu.

Kiongozi wa mkutano huu alikuwa Prof. Neria De Giovanni, rais wa shirika za kimataifa za Wachunguzi wa Maandishi. Mwandishi wa vitabu 40, baadhi vikiwa kwenye maktaba ya Vatican. Yeye anatoa sauti kwa wanawake kwenye uandishi na historia.

Ilikuwa jioni njema huko Castalplanio, kwenye Kituo cha Kiroho. Pia kulikuwa na chakula kizuri sana kilichoandaliwa na jumuiya na baadhi ya marafiki wa masista; pamoja na biskuti zenye viungo vya Ildagarda, zilizotengenezwa na mwanafunzi wa Kituo. Kulichezwa mziki wa Ildagarda, na Noemi na mwanaye Sara ambao waliikaribisha jioni, wakileta mshangao na amani ya ndani.

Asanteni, wanawake!





**D. Mariano Piccotti**

# Kongamano la Tatu la Watawa Vijana: Huru katika Roho Mtakatifu





Kongamano la Tatu la Watawa Vijana lilifanyika Krakow kuanzia tarehe 13 hadi 16 Septemba, wakikusanyika pamoja washiriki 900 kutoka mashirika 100 ya kike na ya kiume na kutoka taasisi za walei. Mada ilikuwa: Huru katika Roho Mtakatifu. Mikutano mingi ilifanyika katika Kituo cha John Paul II na katika Kanisa la hija la Huruma ya Mungu huko Łagiewniki.

Vijana, uhuru katika Roho Mtakatifu, maneno haya yaliendelea kusikika wakati wa siku za Kongamano na shauku ya washiriki siyo tu ilijaza chumba cha mkutano, bali pia ilitoa uhai nyakati za burudani kama michezo na ngoma.

Padre Krzysztof Wons, SDS, katika mkutano wake wenye kichwa cha habari Roho Mtakatifu anawahakikishia kwenye Maandiko matakatifu ujana wa milele, aliwaelezea ujana wa roho ambao siyo lazima kuhusishwa na tarehe ya kuzaliwa. "Niambie juu ya tamaa zako na nitakuambia kama wewe ni kijana" uhakika huu unaondoa swala la umri na badala yake kuweka kwanza kabisa uwazi kwa Roho Mtakatifu, mawazo yake, ujana wa milele. Padre Krzysztof alizungumzia kuhusu Lectio Divina katika mazingira ya kila siku. Kwa kweli, Neno la Mungu hutufanya sisi kutozeeka na kufa kabla ya kifo.

Mada nyingine muhimu ilikuwa ni uaminifu, ambao, ikiwa tunauishi kila siku, hufanya kutoka katika harakati kubwa kupita kiasi, kutegemea nguvu zetu wenyewe na umotomoto wa nje tu. Sr. Anna Balchan, SMI, Kiongozi wa Chama cha Wanaosaidia Waathirika wa Ukahaba na familia zao, alizungumza juu ya mang'amuzi ya Huruma ya Mungu. Hadithi zake juu ya misaada kwa wanawake wanaoteswa, waliorarulіwa na "Jehanamu" ya unyanyasaji, zilinifanya nijiulize swali: Ninajibuje mwaliko wa Mungu wa kuleta Damu ya Kristo kwa watu waliotengwa? Ushuhuda wa Padre Krzysztof, Sr. Anna na Padre Stanisław Jarosz, OSPPE, umenionyesha kuwa inawezekana na ni vizuri kuishi maisha ya wakfu na Yesu.

Wakati wa Kongamano nilipewa kazi ya liturujia pamoja na Michael. Hii ilikuwa changamoto muhimu sana kwangu, ambapo kupitia kwayo nilitaka uzuri wa liturujia, utajiri wake katika utofauti wa maelezo uonekane.

Katika mpango wa liturujia, Njia ya Msalaba ilikuwa ni mang'amuzi muhimu zaidi kwangu; Niliandaa vituo vingine nikichukua yale yaliyomo katika tasaufi yetu na katika tafakari ya Padre Krzysztof Grzywocz, ambaye aliondoka kwa huzuni kwa sababu ya msiba. Mengine yalifafanuliwa na masista watawa wa Trzebinia. Kumfuata Yesu mpaka Kalvari, ilinisaidia kugundua tena ukaribu wake katika hali ngumu zaidi. Yeye hayuko tofauti nami katika kujaribiwa, ambapo mara nyingi huwa sikubali. Niliguswa na ukweli kwamba mawazo haya kuhusu Njia ya Msalaba yamewasaidia washiriki wengi kuonja wema wa Mungu.

Katika siku hizi huko Krakow tulimwona Mungu kijana, anayependana na mwanadamu. Matukio mengine mawili muhimu ya Kongamano yalikuwa ni matembezi kuelekea katikati ya jiji na tamasha la bendi ya NiemaGot.

Kongamano lilikuwa kwangu shule ya mahusiano, hata matatizo tuliyoyapata yalikuwa si kitu kilichoweza kutufanya kushindwa, bali nafasi ya kujifunza kushirikiana.

***Sr. Tatiana Studentowa, ASC***

# Elimu kwa heshima ya viumbe vyote

Tumepewa maisha ili yaweze kuzaa kikamilifu. Safari ya kiroho ya kumfuata Yesu inahusishwa kwa karibu na miujiza ya kila siku ya neema, lakini pia kwa maajabu ya asili, ambayo aliyaosha wakati wa maisha yake ya duniani: "maua ya shamba", "punje ya ngano" inayoanguka chini na kuzaa matunda. Anaongea juu ya ardhi yenye rutuba na isiyo zaa, juu ya ngano kwenye udongo mzuri na inayosongwa na miiba na inayoanguka kwenye miamba. Papa Francis anaonya kuwa katika ngazi mbalimbali, mara nyingi nchi inamharibu mtu yuleyule na kuzuia maisha na mahusiano "na Mungu, na wanadamu wengine na dunia ... tuna changamoto kubwa ya kitamaduni, kiroho na elimu" (Waraka wa Papa 'Laudato Sì Nambaa 66 na 202).

Kwenye Region ASC ya Zagabria, miezi ya Septemba na Oktoba iliashiriwa na sala na kazi zilizohusu zaidi utamatuni wa mazingira. Sala yenye ubunifu iliandaliwa kwa ajili ya "Siku ya Viumbe vyote" na ilikuwa kama hewa safi kwa karibu jumuiya zote za ASC, Jumuiya ya Damu ya Kristo na jumuiya ya parokia ambazo masista wanafanya utume. Wengi walieleza mangamuzi yao ya sala na walitiwa moyo ili kuwa mfano wa shukrani na kujenga uwiano kati viumbe na mazingira. Kwenye jumuiya zetu litathimini ufahamu wetu juu ya mazingira ili kutumia rasilimali za "nyumba yetu ya pamoja" kwa akili zaidi na kuitunza nchi yetu katika hali ya usafi.



Kazi za elimu zinazofanywa na watoto wa rika zote na mipango ya elimu na katekesi parokiani ziliwekwa katika mada: "Kwa pamoja kujenga na kuandaa ulimwengu", "Amsha ndani yako "mazingira" na mengineyo.

Utendaji ulihusisha utengenezaji wa mazingira, utenganishaji wa taka, utengenezaji wa vitu vinavyofaa kutumia kutoka kwenye chupa za plastiki, uokotaji wa nyuzi zilizotumika, na uzalishaji wa kapeti na mikoba, kuchakata karatasi ili kutengeneza vitabu vya kufundishia, upandaji wa maua kwenye bustani ya shule, uchuchaji ya maji, matumizi bora ya maji na chochote kila ambacho kilikuwa kimetengenezwa, pamoja na mahusianao mazuri ya pande zote ambayo ni muhimu kwa afya, amani na furaha.

Inashangaza jinsi watoto walivyofikia hitimisho kwamba hakuna viwanda vya misitu, milima na bahari, na kama misitu inaharibiwa, mbwa mwitu, vicheche na wanyama wengine hawataweza kuishi, mada hii iliwasukuma kufikiri juu ya wajibu wao kwa hewa, ardhi, maji, ulimwengu na mimea na wanyama na taji la uumbaji: mtu.





Katika kuongea juu ya hekima ya Mungu na wema wake ambapo aliumba ulimwengu, waligusia pia juu ya mada ya mazingira. Katika masimulizi ya uumbaji (Mwanzo 2), waliyoyachukua kama msingi kwa tafakari, walitambua " utume wa kwanza na wa kudumu wa binadamu": kulima na kuitunza ardhi (rejea Mwa. 2:15). Kuhimizana wao kwa wao na kuwahimiza wengine juu ya umuhimu wa amri hii ya Mungu na wajibu wa mwanadamu, wanafunzi wa shule ya msingi DavorinTrstenjak ya Zagabria pamoja na Sr. Marija Bilanović, wakati wa vipindi vya dini, walifanya jaribio "Namna gani vitu vinaharibu ardhi" "vitu vinne vilifukiwa kwenye shamba la shule, karatasi za kufutia mdomo, bilauri ya plastiki, na kipande cha kioo na kipande cha chuma.  Vitu vilivyofukiwa vitabaki chini ya ardhi hadi siku ya kimataifa ya Mama Ardhi 22 Aprili 2019.

Hivyo watagudua vitu na wataandika watakachoona na watatoa hitimisho ambalo litawasilishwa kwa wanafunzi wengine wa madarasa ya chini kwa mtindo wa kuwatangazia kwa kubandika karatasi za matangazo au kwa mtindo wa kutumia Power Point.

Adhimisho la Misa Takatifu ya siku ya Shukrani ya mavuno ya ardhi iliandaliwa kwa ubunifu mkubwa. Shughuli zote hizi zinatusaidia sisi



kufungua macho yetu kuona vizuri kazi kuu za Mungu katika maisha yetu na katika watu, katika viumbe vyote na kujenga tabia ya uwajibikaji kwa mazingira ya asili, ambamo Mungu alituweka kwa  upendo Wake.

***Sr. Cecilija Milković, ASC***

## Kalenda ya Uongozi Mkuu




**6 Januari:** Nyumba Kuu – Tamasha la nyimbo kwa ajili ya Epifania: Usiku wa upendo kufuata nyota

## *Sherehe za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha ya*

| | | |
|---|---|---|
| miaka 40 | | |
| **Sr. Theresia Rogatus Mwimba** | 08/01/1979 | Tanzania |
| miaka 50 | | |
| **Sr. Ra Mi Agnes Yoon** | 02/01/1969 | Corea |
| miaka 60 | | |
| **Sr. Sônia Maria Pinho de Matos** | 04/01/1959 | Manaus |
| miaka 70 | | |
| **Sr. Sue Andrew** | 06/01/1949 | USA |
| **Sr. Maria Grazia D'Amato** | 14/01/1949 | Italia |
| **Sr. Francisca Lafuente Hidalgo** | 23/01/1949 | Spagna |
| **Sr. Bernarda Krištić** | 24/01/1949 | Zagreb |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Teresa Cardetta** | 08/01/1939 | Italia |
| **Sr. Giuseppina Pacifico** | 12/01/1939 | Italia |
| **Sr. Maddalena Orsillo** | 26/01/1939 | Italia |
| miaka 90 | | |
| **Sr. Attilia Compagno** | 01/01/1929 | Italia |
| **Sr. Frances Newton** | 16/01/1929 | USA |
| **Sr. Mary Peter Chiodo** | 19/01/1929 | USA |





## *Waliorudi Nyumbani kwa Baba*

| | | |
|---|---|---|
| 12/12/2018 | **Sr. Rita Pace** | Italia |
| 16/12/2018 | **Sr. Bernardina De Angelis** | Italia |
| 17/12/2018 | **Sr. Luigina Pace** | Italia |


**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*

...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 1, Januari 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*